BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 15 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 16 Disemba, 2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2022/2023.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

121. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Lengo kuu la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) ni kusaidia kuleta maendeleo ya majimbo 50 ya Zanzibar. Sheria hiyo pia inazuia baadhi ya matumizi kwa maendeleo hayo ikiwemo ukarabati wa barabara za ndani kwa kuweka na kushindilia vifusi hata kama lengo ni kupunguza kero kwa wananchi.

Je, Serikali haioni haja ya kuirekebisha Sheria hii kwa lengo la kusaidia kupunguza baadhi ya kero kwa wananchi, ikiwemo kuhalalisha ukarabati wa njia za ndani kwa kuweka na kushindilia vifusi.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

142. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa muda mrefu sasa suala la ziwa maboga limekuwa likija Barazani kwenye mijadala ya ripoti mbali mbali za Kamati na Bajeti za Serikali, na mara ya mwisho Serikali imetoa taarifa kuwa kuna mradi wa Big Z utashughulikia athari za kimazingira za ziwa maboga na makubaliano yameshafanyika kwa hatua za awali. Hata hivyo, bado ziwa maboga linaendelea kuleta athari kwa wananchi na kila mwaka watu wanapoteza maisha, na hivi karibuni tu kuna mtoto mdogo amepoteza maisha.

(a) Je, ni hatua gani ya utekelezaji iliyofikiwa hivi sasa, ya kuondoa athari za kimazingira katika ziwa maboga.

(b) Kwanini Serikali inachukuwa muda mrefu kulishughulikia ziwa maboga na huku kila siku zikienda linazidi kuleta athari kwa wananchi ikiwemo vifo.

(c) Kwa kuwa jambo hili limeshakuwa la muda mrefu sana. Je, ni upi mkakati wa kulimaliza kabisa tatizo la ziwa hilo ili wananchi wa eneo la ziwa maboga waishi kwa amani.

**Ofisi ya Rais, Ikulu:**

106. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Tumekuwa tukijionea kupitia awamu mbali mbali zilizopita Marais wetu wanapo safiri kwenda nje ya nchi kusafiri pamoja na watendaji mbali mbali wakiwemo Mawaziri na baadhi ya Wawakilishi wa kawaida kwa lengo la kuitumia fursa hiyo kupata kujifunza mambo mbali mbali kutoka kwa wenzetu huko

(a) Je, katika awamu hii ya nane hadi sasa Rais wetu ameshafanya ziara ngapi za nje ya nchi.

(b) Je, ni Wawakilishi wangapi wamepata fursa ya kufuatana na Mhe. Rais kupitia ziara hizo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

21. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna baadhi ya vituo vya daladala Zanzibar miundombinu na mazingira yake hayapo kwenye hali nzuri. Miongoni mwa vituo hivyo ni pamoja na kituo cha Uwanja wa Ndege.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuviwekea miundombinu na mazingira mazuri vituo vyenye changamoto hizo ili kuepusha madhara tofauti yatokanayo na changamoto hizo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

37. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa muda wa miaka miwili hivi, skuli nyingi zimekuwa na upungufu wa walimu hasa wa skuli za msingi. Kwa bahati njema, hivi sasa vijana wengi wanasomea fani hii ya ualimu kwa ngazi ya Diploma.

(a) Je, ni lini Wizara yako itaajiri walimu kwa mahitaji ya skuli husika.

(b) Je, kwa nini walimu wengi wanaoajiriwa ni vijana kutoka mjini na mahitaji ya walimu hao yanahitajika katika skuli za shamba.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

26. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR HASSAN (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Tume ya Utangazaji inakabiliwa na changamoto ya kukosa jengo la ofisi ambapo imelazimika kukodi jengo kwa gharama kubwa kwa upande wa Unguja.

(a) Je, Wizara ina mpango gani katika kutatua changamoto hii.

(b) Je, ni kiasi gani cha kodi kinacholipwa kwa mwaka.

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kama tulivyowahi kushuhudia katika Baraza hili, Serikali yetu iliruhusu rasmi Mchezo wa Ngumi hapa Zanzibar, hali iliyowapelekea wananchi kuwa na matumaini kuwa, hivi sasa nchi yetu itashuhudia mashindano ya mchezo huo Kitaifa na Kimataifa yakifanyika hapa nchini.

(a) Je, hatua za kuusajili rasmi Mchezo wa Ngumi na kuuridhia hapa Zanzibar zimefikia wapi.

(b) Je, ni changamoto zipi mpaka sasa ambazo zinapelekea kuchelewesha usajili wake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

7. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya njia kongwe Chake - Wete imekuwa ikijengwa kwa mwendo wa pole pole na inatakiwa ikabidhiwe Serikalini katika kipindi cha miezi thelathini (30) tokea kuanza kazi ya ujenzi wa njia hiyo.

Je, ujenzi huo ulikamilika kwa asilimia ngapi mpaka kufikia mwezi wa Oktoba mwaka wa 2022.

105. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kulikuwepo na utaratibu wa barabara zetu kukatwa majani pembezoni mwa barabara ili kuziweka safi barabara hizo.

(a) Je, utaratibu ule umeondoka kwa sasa.

(b) Kama haujaondoka, kwa nini barabara nyingi kwa sasa hazifanyiwi usafi huo.

152. MHESHIMIWA AZZA JANUARI JOSEPH (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Imekuwa ni kawaida kwa wasafiri wanaokwenda Tanzania Bara na kurudi Unguja, kuuziwa tiketi kwa bei ya juu kwa kisingizio kuwa tiketi zimeisha.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inalifahamu suala hili.

(b) Je, ni sababu gani zinazosababisha kiwango cha fedha anayoilipa abiria ikawa ni tofauti na ile inayosomeka katika tiketi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

17. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kila mwaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo hufanya maonesho ya siku ya chakula katika kisiwa cha Pemba katika kijiji cha Kiuyu eneo la Chamanangwe. Kwa kuwa maonesho haya yamekuwa na mvuto mkubwa kwa wajasiriamali katika sekta mbali mbali, na kwa kuwa usafiri umekuwa ni tatizo katika maeneo hayo, hali inayosababisha ajali na majeruhi pamoja na vifo vya wananchi.

Je, ni lini Serikali itanusuru maisha ya wananchi wake kwa kufanya maonesho haya Kiwilaya, ili kupunguza ajali na msongamano usiokuwa na haja.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

4. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wakati Wizara ya Maji, Nishati na Madini inaendelea na zoezi la ukarabati wa kuweka miundombinu mipya ya mabomba ya maji na kuondoa ile ya zamani, bado kuna changamoto ya kuharibika miundombinu hiyo ya zamani na kupotea kwa vielelezo mbali mbali vya kihistoria katika miundombinu hiyo.

(a) Je, Wizara inatambua kwamba miundombinu ya zamani ya tokea ukoloni ni sehemu ya vielelezo muhimu vya historia ya nchi yetu.

(b) Je, Wizara inashirikiana vipi na wataalamu wa Mambo ya Kale katika kufanya “Heritage Assessment” kabla na wakati wa zoezi hilo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

70. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Moja ya kazi za Ofisi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar, ni kusikiliza madai mbali mbali ya wananchi yanayohusiana na mirathi. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya madai mengi yanayofikishwa hapo kutofikia muwafaka mzuri na wananchi wengi wenye madai hayo hatimae hufungua kesi za mirathi katika Mahakama ya Kadhi.

(a) Je, ni ugumu gani unaojitokeza katika ushughulikiaji wa madai hayo katika Kamisheni ya Wakfu.

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kukosekana kwa maamuzi ya familia ambayo yatarahisisha kumfanyia wepesi mrithiwa.

(c) Je, ni mara ngapi Kamisheni hutoa elimu kuhusiana na mirathi ukiachia ile wiki ya maadhimisho ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

27. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kipindi cha muda mrefu Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imekosa kuwa na Sera yake ya Mambo ya Kale, ingawa tumepata taarifa kuwa, hivi sasa Sera hiyo ipo katika mchakato wa kutayarishwa.

(a) Je, kukosekana kwa Sera ya Mambo ya Kale kumeiathiri kwa kiasi gani Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

(b) Je, mchakato wa kuwa na Sera ya Mambo ya Kale umefikia hatua ipi hadi hivi sasa.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2022/2023.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
15 Februari, 2023. KATIBU WA BARAZA.